

COMPANY HIGHLIGHT

HIGHLIGHTS

# Soko la Mitiki India

by Sid Bhargava- Mwakilishi KVTC India

Mbao za mtiki ni maarufu na zinapendwa sana India. Hi ni kwasababu India ilikuwa na bado wana Mitiki mingi na mizuri na wako karibu na Mynamar ambako pia wanalima mitiki bora sana.

Kwasasa India inaagiza mitiki zaidi ya mita za ujazo 100,000 kwa mwezi kutoka sehemu mbali mbali duniani. Kupungua kwa misitu na kuongezeka mahitaji ndio sababu inayoongeza uagizaji mbao za mitiki. Soko la India linachukua zaidi ya 80% mita za ujazo ya mitiki yote duniani na asilimia 75 kwa thamani. India inapendelea kununua magogo au mbao zilizochanwa kwa mraba kutokana na kutokuwa na uwiano wa vipimo ndani ya nchi. Kwa kufanya hivyo kodi huwa nafuu pia.

America ya kusini (Brazil, Ecuador, Costa Rica, Panama and others) ndio wauzaji wakubwa wa mitiki ikifuatiwa na Africa (Ghana, Benin, Nigeria, Tanzania na Sudan kusini, Ivory Coast) halafu Myanmar. Mitiki inatumika zaidi kutengeneza fanicha , milango, madirisha , frame za madirisha na sakafu.

India ina watu bilioni 1.3 na wenye kipato cha kati wanaongezeka hivyo ni soko linalokuwa kwa kasi. Hata hivyo kunachangamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na:

- Mbao zisizo na ubora zinaingia kwenye soko na kuipa mitiki sifa mbaya
- Matumizi ya malighafi mbadala kutengeneza fanicha, milango na frame
- Kuna mapokeo mabaya ya kuona matumizi ya mbao ni mabaya kimazingira.
- Makubaliano ya pamoja kati ya shirikisho la mbao ngumu America na Canada kuhamasisha matumizi ya mbao za Walnut, Oak na Ash.
- Kuongezeka kwa gharama za uzalishaji ambazo zinaleta madhara pia kwenye mbao



Pamoja na changamoto zote hizi pia kuna fursa zifuatazo:

- Kuwa na mbao zenye ubora.
- Kujenga uhusiano na wanunuzi na kuuza mbao kutokana na mahitaji yao ikiwa ni pamoja na mbao zilizokaushwa vizuri.
- Ujenzi na nyumba zitaendelea kuhitajika kwa muda mrefu hivyo kutakuwa na hitaji la mbao.
- Kipato kinaendelea kuongezeka hivyo mahitaji ya mbao zenye ubora yataendelea kuwepo.

Soko la mitiki la India litaendelea kukua na wauzaji watakaoweza kujenga mahusiano mazuri na wanunuzi na kuwa na bidhaa bora wataendelea kupata fursa nzuri ya biashara



KVTC inauza kwenye soko la India zaidi ya miaka 10 sasa na imeweza kuwapatia wateja wake bidhaa nzuri na zenye ubora kutokana na matakwa yao. KVTC inafanya biashara na wasafirishaji kwenda njee, wauzaji, watengenezaji bidhaa za mbao na wenye viwanda vya mbao vinavyotengeneza bidhaa mbali mbali. Mbao za KVTC zinatumika kwenye matumizi mbali mbali kama moldings, beading, fanicha, frame za milango na madirisha, milango, madirisha, ubao unaotokana na vipande vilivyounganishwa na vipande kwajili ya sakafu. KVTC inauza kwenye soko hili moja kwa moja na pia kwa kupitia madalali.



# Kutoka Dawati la Irvine

by Irvine Kanyemba,

Muda unakwenda haraka hasa pale unapokuwa unafurahia unachofanya.

Tunazindua tena mashindano ya kuandika Insha. Mashindano yatawashirikisha wanafunzi wa secondary zilizopo kwenye bonde la Kilombero. Vijana duniani na hata bonde la Kilombero kwa ujumla wanajali juu ya mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira vinavyoendelea duniani. Hivyo basi mada ya mwaka huu inalenga huko: Kutokana na ushahidi wa kisanyansi na tunayoyashuhudia kwa macho, ni kweli mabadiliko ya tabia nchi yapo na yanaendelea kutokea, Mabadiliko haya yanamadhara gani kwenye bonde la Kilombero? Nini suluhisho na njia ya kukabiliana na mabadiliko haya? Tutachapisha matokeo ya Insha kwenye jarida lijalo December 2019

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Njee ya Finland imetoa mchango wa euro za ulaya 164,351 (Zaidi ya TZS 400million) kuendeleza programu ya upandaji miti ya wakulima wa njee kwa mwaka 2019-2020. Hii itawezesha kampuni kuendeleza programu hii ya wakulima wa njee kwa kiwango kikubwa. Maombi yameanza kupokelewa na karibu watu 200 wamefanya maombi. Kutakuwa na upendeleo maalumu kwa watu wenye chagamoto za kimaumbile, wasiojiweza na kinamama.

Tunapenda jarida hili liwe pia kuhusiana na wadau wetu. Utaanza kuona tukiandika makala kutoka kwa wadau wetu mbali mbali kuanzia kwenye toleo hili.

Pia tungependa kusikia kutoka kwa waanzilishi wa KVTC. Tafadhali tuandikie kwa barua pepe ikanyemba@kvtc-tz.com. Tungependa kujua uko wapi na unajishughulisha na nini. Ingekuwa vizuri kusikia na kuandika kuhusu waanzilishi.



Bidhaa zetu bado zinahitajika sana pamoja na uchumi wa India kuyumba kidogo. Tunategemea kuhudhuria maonyesho ya kibiashara ya ndani na njee ya Tanzania mwakani na mbeleni. Kwa niaba ya familia ya KVTC niwatakie sikukuu njema ya DIWALI

# Miradi Maendeleo

by **Sauti ya Wanufaikaji**

Mradi wa maendeleo jamii wa KVTC unaendelea kufanya kazi na vijiji husika. Kipaumbele ni maeneo ya elimu, maji, afya na kujenga uwezo. Kwenye makala hii tunaongea na wanufaikaji wa miradi hii. Shule ya Msingi Milola ni wanufaikaji wa mradi wa maendeleo ya jamii wa KVTC. Shule inawanafunzi 1000 na madarasa 8 ikiwa ni uwiano wa 1:125 lakini kiwango sahihi ni uwiano wa 1: 45, hivyo kunauhaba wa madarasa ukiachilia mbali changamoto nyingine

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Milola Bwana Lusajo anafurahishwa sana na matokeo ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa kupitia kijiji cha Milola kwa kushirikiana na KVTC na kufika mpaka shuleni. "*Kuuingiza umeme shuleni na kupewa computer na mashine ya kutolea nakala kwa kupitia KVTC kulibadilisha hali ya shule na maisha kwa ujumla.*



*Bwana Lusajo (kushoto) wakati wa Ujenzi wa Madarasa awamu ya pili Milola*

*Mashine ya kutolea nakala (fotokopi) imeongeza idadi ya majaribio na mitihani inayotolewa kwa wanafunzi. Hii pia imeleta usawa maana wazazi hawahitajiki tena kuchangia gharama za mitihani kama awali. Hapo kipindi cha nyuma, wakati mwingine mwanafunzi zaidi ya mmoja wanalazimika kutumia karatasi moja ya mtihani au mwalimu kulazimika kutumia chaki kuandika mitihani ubaoni kitendo ambacho kinatumia muda mwingi hivyo majaribio hayakuwa yakitolewa mara kwa mara na mara nyingi kutokufanyika kabisa.*

Bwana Adolf Izoba Mushirizi (picha ya juu kabisa) ni mwalimu Mkuu shule ya Igumbiro, mmoja kati ya watu wa awali kabisa waliopokea huduma ya umeme shuleni, kompyuta na mashine ya fotokopi kwa kupitia KVTC. Bwana Adolf anasema: *Matokea ya mitihani kiwilaya yamekuwa bora, kutoka 82 kati ya 92 mwaka 2014 mpaka kufikia number*

Bwana Salum Mvogo, Mwenyekiti wa Kijiji Milola pia anaelewa umuhimu wa mfuko huu wa maendeleo ya jamii na ambavyo umekuwa kichocheo na kigezo cha kupata pesa za maendeleo kutoka serikali kuu. *Serikali kuu ina utaratibu kwamba kijiji kikianzisha mradi wa darasa na kujenga mpaka kiwango cha lenta basi serikali itatoa pesa za kumalizia. Serikali ya Kijiji Milola ilianza ujenzi wa madarasa mawili na office kwa kutumia fedha shillingi 5million za maendeleo jamii kutoka KVTC, ambayo ilifanya serikali ijazie shillingi 37,510,000 baada ya kuona juhudi za kijiji kwenye hili.*

Rehema Nyoka ni mratibu elimu shule ya msingi Ulanga anaelezea kwamba: *Mfuko wa maendeleo jamii wa KVTC umesaidia kuboresha matokeo ya shule kiwilaya. Shule ilishikilia nafasi ya 39 mwaka 2017 mpaka nafasi ya 5 mwaka 2018 kwenye halamashauri 186.*

**TUSIKILIZE RADIO PAMBAZUKO**

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM
Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi

**WASILIANA NASI AU TUANDIKIE**

kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/
PO Box 655, Ifakara, TZ
PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ